

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA TATU

YATOKANAYO NA KIKAO CHA THELATHINI NA TATU

31 MEI, 2016

MKUTANO WA TATU - YATOKANAYO NA KIKAO CHA THELATHINI NA TATU

TAREHE 31 MEI, 2016

I. DUA:

Saa 3.00 Asubuhi Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) alisoma Dua na Kuongoza Bunge.

Makatibu Mezani:

1. Ndg. Thomas Kashililah
2. Ndg. John Joel
3. Ndg. Ramadhan Issa
4. Ndg. Asia Minja

II. KIAPO CHA UAMINIFU:

Mhe. Jaku Hashim Ayoub aliapa Kiapo cha Uaminifu.

III. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

1. Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Mfuko wa Bunge na Mfuko wa Mahakama kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
2. Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.
3. Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama juu ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka 2015/2016 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2016/2017.
4. Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mwasilishaji wa Kambi ya Upinzani wakati wa kuwasilisha alitumia neno Ndugu Naibu Spika kiti kilimuelekeza kufuata Kanuni na alitumia neno Mheshimiwa Spika na mara baada ya kuwasilisha alitoka nje ya Ukumbi wa Bunge.

IV. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa:-

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na.266 – Mhe. Amina Saleh Mollel [kny. Susan Anselm Lyimo]

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Amina Saleh Mollel

(ii) Mhe. Edward Franz Mwalongo

(iii) Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma

Swali Na.267 – Mhe. Rashid Mohammed Chuachua

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Rashid Mohammed Chuachua

(ii) Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na.268 – Mhe. Josephine Johnson Genzabuke

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Josephine Johnson Genzabuke

(ii) Mhe. Abdallah Hamisi Ulega

(iii) Mhe. Ritta Enespher Kabati

(iv) Mhe. Juliana Daniel Shonza

Swali Na.269 – Mhe. Musukuma Joseph Kasheku

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Musukuma Joseph Kasheku

(ii) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi

(iii) Mhe. Venance Methusala Mwamoto

(iv) Mhe. Constantine John Kanyasu

WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

Swali Na.270 – Mhe. Almas Athumani Maige

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Almas Athumani Maige

(ii) Mhe. Munde Tambwe Abdallah

WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:

Swali Na.271 – Mhe. Mariam Nassoro Kisangi [kny. Dkt. Faustine Ndugulile]

Swali la nyongeza: Mhe. (i) Mhe. Mariam Nassoro Kisangi

(ii) Mhe. Keissy Ally Mohammed

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

Swali Na.272 – Mhe. Ritta Enespher Kabati [kny. Upendo Furaha Peneza]

Swali la nyongeza: (i) Mhe. Ritta Enespher Kabati

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Swali Na.273 – Mhe. Stanslaus Haroon Nyongo [kny. Mhe. Lolesia Jeremiah Bukwimba]

Swali la nyongeza: (i) Stanslaus Haroon Nyongo

MATANGAZO:

- Wageni wote walioko kwenye *galleries* walitambulishwa Bungeni wakiwemo Mabalazi wanaowakilisha nchi mbalimbali na Wabunge wa Afrika Mashariki.
- Kamati ya uongozi ilitangazwa kukutana saa 7.00 mchana
- Kampuni ya Uswisi ya kutoa chumvi kwenye Maji ya Visima itakuwepo Nyerere Square.

MWONGOZO WA SPIKA:

Mhe. Musukuma Joseph Kasheku aliomba Mwongozo kwa kutumia Kanuni ya 68(7) alitaka kujua kama Wabunge wanatakiwa kuwatumikia Wananchi au kusaini na kuondoka. Kiti kilitoa maelekezo kwamba jambo hili lilishatolewa mwongozo siku za nyuma na Wabunge wote wanatakiwa kufanya kazi siyo kusaini na kuondoka. Pia kama jambo hilo linahusu Kambi ya Upinzani ambao hawapo watawala waliangalie.

Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa alitaka kujua tofauti ya Kiapo cha Uaminifu kati ya Serikali na Bunge kwamba Wabunge wanamalizia kwa kusema “kwa mujibu wa Sheria iliyowekwa” wakati Serikalini wanamalizia kwa kusema “iliyowekwa kwa Mujibu wa sheria” na kutaka waliokosea waape upya kwa vile kiapo ni cha muhimu. Kiti kilielekeza kutolea maelezo baadaye mwongozo huo.

V. HOJA ZA SERIKALI:

- Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki aliwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na alitoa hoja ambayo iliungwa mkono.
- Mhe. Kanali (Mst) Masoud Ali Khamis aliwasilisha maoni ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mjambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka 2016/2017.

- Mhe. Mch. Peter Simon Msigwa aliwasilisha Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka 2016/2017.
- Baada ya Mhe. Mch. Msigwa kumaliza, kiti kilitoa mwongozo kuwa maneno yaliyopo uk.32, paragraph ya mwisho yaondolewe na yasiwe sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge kwani ni ya kichochezi na ya kuudhi kwa mujibu wa kanuni za Bunge. Uamuzi huo ulitolewa kwa mujibu wa kanuni ya 5 ya kanuni za Bunge.

Mjadala wa Jumla

Wabunge wafuatao walichangia:-

- | | | |
|------------------------------------|---|-----|
| 1) Mhe. Livingstone Joseph Lusinde | - | CCM |
| 2) Mhe. Stephen Julius Masele | - | CCM |
| 3) Mhe. Cosato David Chumi | - | CCM |
| 4) Fakharia Shomar Khamis | - | CCM |
| 5) Mhe. Jaku Hashim Ayoub | - | CCM |

VI. KUSITISHA BUNGE:

Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni.

VII. BUNGE KUREJEA:

- Saa 10.00 Bunge lilirejea na kuongozwa na Mwenyekiti, Mhe. Najma Murtaza Giga. Majadiliano yaliendelea na wafuatao walichangia Mjadala wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

- | | | |
|--|---|---------|
| 6. Mhe. Joseph Osmund Mbilinyi | - | CHADEMA |
| 7. Mhe. Joseph Kasheku Musukuma | - | CCM |
| 8. Mhe. Masoud Abdallah Salim | - | CUG |
| 9. Mhe. Raisa Abdallah Mussa | - | CUF |
| 10. Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa | - | CCM |
| 11. Mhe. Masoud Ali Khamis | - | CCM |
| 12. Mhe. Mattar Aly Salum | - | CCM |
| 13. Mhe. Allan Joseph Kiula | - | CCM |
| 14. Mhe. Balizi Adadi Rajab | - | CCM |
| 15. Mhe. Daniel Nsanzugwanko | - | CCM |
| 16. Mhe. Lucy Simon Magereli | - | CHADEMA |
| 17. Mhe. Hamidu Hassan Bobali | - | CUF |
| 18. Mhe. Khatib Said Hajji | - | CUF |
| 19. Mhe. Nagenjwa Livingstone Kaboyoka | - | CHADEMA |

- | | | |
|--------------------------------|---|---------|
| 20. Mhe. Emmanuel Papian John | - | CCM |
| 21. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha | - | CUF |
| 22. Mhe. Susan Anselm Lyimo | - | CHADEMA |
| 23. Mhe. Goodluck Asaph Mlinga | - | CHADEMA |
| 24. Mhe. Khadija Hassan Aboud | - | CCM |
| 25. Mhe. Hafidh Ali Tahir | - | CCM |
| 26. Mhe. Mohammed Ally Keissy | - | CCM |
27. Mhe. Dkt. Merdad Matogolo Kalemani – Naibu Waziri wa Nishati na Madini.
28. Mhe. January Y. Makamba – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).
29. Mhe. Harrison George Mwakyembe – Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.
30. Mhe. Dkt. Augustine Philip Mahiga – Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

KAMATI YA MATUMIZI:

Bunge liliingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi ili kupitisha Vifungu vya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Baada ya kumaliza, Bunge lilirejea, Waziri Mtoa Hoja alitoa Taarifa ya Kazi ya Kamati, Wabunge walihojiwa na kupitisha Bajeti husika.

TAARIFA YA SPIKA:

Kiti kilitolea ufafanuzi mwongozo wa Mhe. Victor Mwambalaswa kuhusu maneno ya kiapo kutofautiana maneno kati ya Serikali na Wabunge kwamba ni kwa mujibu wa *The Official Oaths Acts* ni maneno yaliyotumia na kuapa na Wabunge kwa hiyo kiapo cha Wabunge ni sahihi.

VIII. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE:

Saa 2.25 Usiku Bunge liliahirishwa hadi tarehe 1/6/2016 saa 3.00 asubuhi.

DODOMA
31 MEI, 2016

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE